SOMO LA 12

WAJIBU NA HUKUMU

“Na wote waliokosa, wenye sheria, watahukumiwa kwa sheria” (Warumi 2:12-16)

UKRISTO WA JADI UMEFUNZA - na waendelea kufunza dhana ya kusema kuwa wanadamu huzawadiwa (au kuadhibiwa) mara wanapokufa kwa kupelekwa mbinguni au motoni (hell); na baada ya miaka kadhaa baadaye, wakisharudishwa wataingia miili yao ya kufa na wasimame mbele ya Kristo kwa hukumu ili kubaini ijara (au adhabu) wanayostahili.

Masomo haya yameonyesha mara nyingi ya kuwa ujumbe wa Mungu uliomo katika Biblia ni wa kimantiki na thabiti; changamoto hapa ni mtu aonyeshe mantiki au uthabiti ulioko katika nadharia hiyo ya ukristo wa jadi. Ikiwa kifo yaendeleza uhai hasa, na ya kuwa zawadi yapatikana na kupokelewa kwa njia hiyo, sasa wapi mantiki katika mafunzo ya maandiko kuhusu Siku ya Mwisho ya ufufuo na siku ya mwisho ya hukumu?

Hata hivyo, maandiko yanatupa picha iliyo wazi, inayoonyesha wafu hawajui jambo lolote, bali wanalala kabisa bila ufahamu makaburini mwao, wakisubiri Kristo awaite na kuwapa uhai katika miili yao kwa njia ya ufufuo ili wapate kuhukumiwa, HALAFU wapate malipo. Hii ni maridadi, inayofanana na tena yafaa.

SIO WOTE WATAFUFUKA KUTOKA KWA WAFU

Mungu hatawaleta wanadamu wote ili wakuhukumiwe. Wengi wa wanadamu wako katika kundi ambalo zaburi 49 linaelezea –

“Lakini mwanadamu hadumu katika heshima, bali amefanana na wanyama WAPOTEAO… Kama kondoo wamewekwa kwenda kuzimu … Usiogope mtu atakapopata utajiri, maana atakapokufa hatachukua chochote … Atakwenda kwenye kizazi cha baba zake … Hawataona nuru hata milele. Mwanadamu mwenye heshima, iwapo hana akili, amefanana na wanyama WAPOTEAO ” Hivi ni vizuri na haki. Kuwaleta watu wasiojielewa kwa hukumu kwa sheria ambayo hawakuielewa si jambo zuri.

HUKUMU NI KWA MISINGI YA WAJIBU

Hukumu msingi wake ni wajibu. Wajibu wetu kwa Mungu inatokana na mawasiliano yetu na sheria yake, uwezo wetu wa kuelewa mema na uovu, na uwezo wetu wa kuthibiti matendo yetu kulingana na ufahamu huu. Biblia ndiyo chanzo cha pekee cha ujuzi mwafaka kuhusu kanuni na matakwa ya wajibu mbele za Mungu. Falsafa na nadharia za wanadamu ni bure kabisa.

ADAMU ALIANGUKA … MPANGO WA MUNGU WA UKOMBOZI

Adamu alikuwa ana wajibu kwa vitendo vyake kwa sababu angeweza kuthibiti vitendo hivyo na aliambiwa cha kufanya. Aliasi akijua, na sheria ya Mungu ikamhukumu. Yeye pamoja na vizazi

vyake wamekuwa chini ya nguvu za dhambi na mauti tangu wakati huo. Lakini Mungu hakutaka kusudi lake la kuujaza ulimwengu huu kwa utukufu ukome kwa kushindwa kwa mwanadamu. Kwa rehema yake kuu, na wema wake alibuni na anashughulikia mpango wa wokovu kwa mwanadamu, huku akihifadhi na kuendeleza heshima yake na utakatifu na haki; sheria kuhusu kutukuzwa Mungu juu mbinguni na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia. Mpango huu wa ukombozi; ambao umeonyeshwa katika Biblia kupitia kwa ahadi kadhaa, amri za sheria, zilifungua tena uhusiano kati ya Mungu na mwanadamu, na ikamfanya mwanadamu ayatafute maadili yakumfanya awe na wajibu kwa Mungu tena.

Ni kanuni ya Mungu kuwa matokeo haya ni kwa wale tu ambao wanafikia upeo wa sheria za Mungu. Wale wasiofikia wako katika kundi la zaburi 49 (tumenukuu hapo juu).

NURU (UJUZI) HUSABABISHA WAJIBU

Mtume Paulo alisema hivi katika waraka kwa warumi –

“Pasipokuwa sheria, hapana kosa” (Warumi 4:15).

Na wale wa Athene aliwaambia:

“Zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni.” (Matendo 17:30)

Kristo alimfahamisha Nikodemu –

“Na hii ndiyo (msingi wa) hukumu (krisis), ya kuwa nuru imekuja ulimwenguni, na watu wakapenda giza kuliko nuru” (Yohana 3:19)

Kwa wayahudi waliomkataa alisema, “Kama mngekuwa vipofu (wajinga) msingekuwa na dhambi ” (Yohana 9:41).

Maandiko yanalinganisha “nuru” kama sababu ya wajibu na ufufuo kwa hukumu – “Basi yeye ajuaye kutenda mema, wala hayatendi, kwake huyo ni dhambi.” (Yakobo 4:17)

“Maana ingekuwa heri kwao, kama wasingalijua njia ya haki, kuliko kuijua, kisha kuiacha ile amri takatifu waliyopewa” (2 Petro 2:21)

“Na kama nisingalikuja na kusema nao, wasingalikuwa na dhambi; lakini sasa hawana udhuru (sababu - vazi) kwa dhambi zao” (Yohana 15:22).

Chini ya sheria ya Musa, ambayo Paulo anainukuu kama mfano – “Kila kosa na uasi ulipata ujira wa haki.” (Waebrania 2:2)

Wale ambao amri hii iliwafikia hawakuulizwa kama walikuwa tayari kutii amri ya Musa. Waliambiwa, waliamriwa. Sawa na wakati wa mwanzo wa Adamu: hakuulizwa kama alikuwa tayari kufanya mapatano: aliamrishwa: aliwekwa chini ya sheria kwa mapenzi ya Mungu ; na kulaumiwa kwa kutotii. Twaweza kukubali kuwa maandiko yanaposema hivi, itatendeka; na

twafahamu haitokei katika siku zetu, haifanyiki, na tunambiwa haitokei (Mhubiri 7:15 ; Ayubu 21:7,13,30).

Watu wakiwa katika hali ya kutojua, haihesabiwi kuwa na wajibu kwa matendo yao, kwa hivyo haajibikii hukumu kama mtu ajuaye. Mungu hupuuzilia (hujifanya haoni) matendo yao, kama vile anavyowachukulia wanyama wa kondeni. Hawana nuru (ufahamu) wala hawana sheria. Wana hali moja na wanyama: kwa ujinga wao wamezama wasiwe na nuru wala wajibu. Ndivyo hali ya wanadamu wengi ilivyo, kama Paulo alivyowambia Warumi… “Kwa kuwa wote waliokosa pasipo sheria watapotea pasipo sheria” (Warumi 2:12)

Kama ni kweli (kama maandiko yasemavyo) waliopewa vingi, vingi vitahitajika, basi ni sawa kutotarajia chochote kutoka kwa yule asiye na chochote. Yesu alisema ya kuwa kama asingalikuja na kusema na kizazi hiki, hakingalikuwa na dhambi, kwa kuwa wangalikuwa na ujinga mwingi (Yohana 15:22). Inakuwa sawa katika kizazi hiki ambao wameitwa kupitia kwa ujumbe wa Injili. Kwa hivyo alisema (Yohana 12:48) –

“Yeye anikataaye mimi, asiyeyakubali maneno yangu, anaye amhukumuye; neno hilo nililonena ndilo litakalomhukumu SIKU YA MWISHO”

Watu hawawezi kuhukumiwa kwa ‘neno’ ambalo hawajawahi kulisikia. Wajibu kwa mwenyezi Mungu hutokana na kujua sheria zake. Kizazi cha Nuhu ni ushahidi mwafaka wa mfano huu. Jamii yake ya karibu ilipokea sheria, walijua na kuifahamu. Na kizazi baada ya kizazi kilipokuja ndivyo ujuzi na ufahamu ulivyowatoka, hata maadili na wajibu ukazama kufikia kiwango cha wanyama, na kusababisha hali ambayo Paulo anasema Mungu alijifanya haoni.

MWITO WA IBRAHIMU – UHUSIANO MPYA

Ibrahimu – baba wa taifa la wayahudi – aliitwa moja kwa moja na kwa uwazi atoke katika giza linalokumba ulimwengu. Mwito huu ulifanya mwelekeo wake wa maisha uwe bora zaidi ya ulivyokuwa alipokuwa katika kiza cha Ukaldayo. Imani na utiifu kwake Mungu ulimfanya awe “mriithi wa ulimwengu” (Warumi 4:13) kwa masharti ya kupata mwili usiopatikana na mauti baada ya ufufuo. Na alipoitwa, kutoamini na kutotii ungemfanya apate adhabu kali yenye matokeo mabaya kuliko yale yaliyomfanya Mungu achukizwe na Adamu.

Paulo aliwaambia Waefeso zamani zile za ujinga “Mlikuwa hamna tumaini, hamna Mungu duniani… wageni wasio na maagano ya ahadi ile …” (Waefeso 2:12).

Mtu anapoitwa kutoka katika hali hii ya kumkosa Mungu kwa kuhubiriwa Injili, wanakuwa mali “yao wenyewe” (1 Kor. 6:19). Shughli zao zote huja chini yake Mungu, na inakuwa chanzo cha kuwajibika kwao siku za mbeleni.

Kama ilivyokuwa kwa upande wa Ibrahimu, wote wanaofikia ufahamu wa ukweli wanakuwa kama yeye alivyowajibika. Sheria ya Imani ilianzia katika Edeni kama tunavyoona katika

Waebrania 11:4 – “Kwa imani Habili alimtolea Mungu dhabihu iliyo bora, kwa hivyo alishuhudiwa ana haki.”

Lakini uanzishaji kamili na rasmi wa Sheria ya Imani kama msingi wa wokovu, ulitokea katika maisha ya Ibrahimu. Huu ndio msingi wa wajibu wa Ufufuo.

Bila shaka, kuna ushahidi ya hali hii kuwepo kabla ya Ibrahimu: Habili, Enoka, Nuhu na kadhalika.

SHERIA YA MUSA ILIFUATILIA: KUSUDI LAKE

Sheria ya Musa ilikuwa msimbo wa kitaifa wa Israeli. Ilikuwa chini ya, na haikuchukua nafasi wala kuipita Sheria ya Imani katika Ibrahimu (ambayo kusema kweli imetokea tangu siku za Habili). Sheria ya Musa ilikuwa ni ya muda mfupi tu ya utawala, iliyoongezwa kwa sababu kadhaa za Mungu, kama:

1. Kuonyesha wanadamu wote ni wenye hatia mbele za Mungu;
2. Kushuhudia ukuu na utakatifu usiokaribiwa;
3. Kuwa kiongozi kutuleta kwa Kristo;
4. Kuwa kivuli, na funzo la mfano wa mambo aina ya yalivyo mbinguni;
5. Kufunika dhambi kwa muda mfupi ili wasamehewe kwa msingi wa utiifu wa kanuni za kutoa dhabihu, na kuwa na imani katika vile vitu vilivyowakilishwa.

Pia ilikuwa msimbo wa kitaifa wa kupanga kudhibiti Israeli kama taifa na ikawa njia ya udhihirisho wake mwenyezi Mungu kwa ulimwengu. Ikawa msingi ambao sheria ya Imani ya Ibrahimu ingeweza kufanya kazi yake kwa ukamilifu.

NAFASI YA SHERIA YA IMANI HAIKUCHUKULIWA; USHUHUDA WA AGANO LA KALE KUHUSU UFUFUO

Sheria ya Musa ilipokuwa ikifanya kazi – ni wazi kuwa kanuni ya wajibu katika ufufuo ilikuwa yafanya kazi pia.

Kanuni imekuwepo tangu siku za Habili hadi za Paulo kupitia kwa yote aliyofanya Mungu kupitia kwa watumishi wake. Kusudi la Mungu kuanzia mwanzo iligusia kazi ya Kristo kama ‘Ufufuo wa Uzima.’

Kristo alisema kuwa Ibrahimu, Isaka na Yakobo na manabii wote watakuwa katika Ufalme wa Mungu (Mathayo 8:11). Mungu alijidhihirisha kwa Musa kupitia kwa Jina la kumbukumbu lilionyesha kanuni ya ufufuo, alipojitaja kama Mungu wa watu waliokuwa taya\\ri wamekufa (Kutoka 3:6). Yesu alitumia kifungu hiki ili kuwanyamazisha Wasadukayo (waliokuwa hawaamini ufufuo) alionyesha kuwa Mungu atawafufua hawa watu tena (Luka 20:37). Twasoma hivi – “Mungu atawahukumu wenye haki na wasio haki; kwa kuwa kuna WAKATI huko kwa kila kusudi na kwa kila kazi (Mhubiri 3:17). “Mungu ataleta hukumuni kila kazi, pamoja na kila

neno la siri." (Mhubiri 12:14). "Basi ninyi msihukumu neno kabla ya WAKATI wake, hata ajapo Bwana; ambaye atayamulikisha yaliyositirika … na kuyadhihirisha mashauri ya mioyo; ndipo kila mtu atakapoipata sifa yake kwa Mungu" (1 Wakorintho 4:5)

"Ndipo wale waliomcha BWANA waliposemezana wao kwa wao… Nao watakuwa wangu, asema BWANA wa majeshi, katika SIKU ile niifanyayo naam, watakuwa hazina yangu hasa… Ndipo mtakaporudi, nanyi mtapambanua kati ya wenye haki na waovu" (Malachi 3:16-18)

Na kuna vifungu vingi vingi vya mfano huu katika maandiko yote ya Agano La Kale (kama vile Zaburi 37; 49:14; 58:10; 62:12 ; Mithali 11:18-31 ; Mhubiri 5:8 ; 11:9; 12 :14 ; Isaya 3:10 ; 26:19-21 ; 35:4 ; 66:4-5,14; Malaki 4:1-3, n.k)

Wajibu wa Wayahudi ulikuwa mkuu kuliko ule wa kizazi cha Nuhu kilichotupiliwa mbali, kwa sababu hawa walikuwa na uhusiano wa karibu na Mungu kama taifa teule kama alivyosema –

"Ni ninyi tu niliowajua katika jamaa zote zilizo duniani, kwa sababu hiyo nitawapatiliza ninyi kwa maovu yenu yote." (Amosi 3:2)

Twaona hapa pia kanuni ya wajibu kwa kuwa na ujuzi. Adhabu waliyopata Wayahudi kitaifa kutoka kwa Waashuru, Wababeli, Warumi na watu wa Mataifa katika karne hizi zote ni matokeo ya wajibu na uamuzi wao wa kitaifa. Na hata hapa kuna ushahidi wa kiwango fulani cha wajibu wa kibinafsi, Kristo aliposema baadhi ya wengine katika kizazi chake wataonyesha majonzi na kusaga meno watakapowaona wale wazee wakikubaliwa katika Ufalme "nanyi wenyewe mmetupwa nje" (Luka 13:28)

MATAIFA MENGINE WANAWAJIBIKA KWA KIASI TU

Kama Waisraeli walivyokuwa na wajibu kiasi na Mungu, twaona kuwa watu wa mataifa mengine yalipokuja kujumuika nao na Mungu wa Israeli, ndipo kiwango cha wajibu wao kilivyopanda. Mataifa ya Amoni, Moabu, Edomu, Wafilistina na Watiro walikuwa **kundi** hili; kama walivyokuwa wale wengine na walipata ghadhabu ya Mungu kwa kiwango cha wajibu wao kwa Mungu. Twaelewa haya kutokana na ushuhuda kama wa Ezekieli 25 – 33, Amosi 1-2, n.k.

Wajibu wa ufufuo ni kwa wale tu walio na ujuzi wa neno la Mungu. Ahadi zake na maagizo yake yanatoa nafasi na kutumika wajibu ikilenga Ufufuo. Yaweka msingi wa kule kuamka kutoka ardhini na kupata uzima wa milele (Danieli 12:2). Kuna ujuzi gani tunaopata kutokana na miaka mingi ambayo imepita ambayo Mungu alijifanya haoni ikiwa mwanadamu yeyote ambaye amewahi kuishi ni "roho isiyokufa" ambayo ni sharti "iokolewe" kwa kugeuzwa au kukubaliwa kuadhibiwa katika moto wa milele? Kwa nadharia hii ya kijinga na potofu isiyo ya kimaandiko, kila mwanadamu aliyewahi kuishi, hata kwa sekunde tu, imempasa kuwepo mahali fulani akiwa hai milele. Ikiwa hawa wamefungwa kuzimu kwa sababu ya ujinga (Waefeso 2:12, 4:18) – haki iliyoje ya Mwenyezi Mungu! Lakini hawa wataruhusiwa kwenda mbinguni katika ujinga wao

kwa kuwa hawajiwezi, hii kazi yote ya kuhubiri injili si ni ukatili mkubwa, inayojenga nafasi nzito ya kukataliwa (Mathayo 7:21 ; 2 Wakorintho 2:14-16), hali ujinga usiosheheni una hakika ya kupata wokovu! Hivi basi nadharia ya jadi ya Wakristo ya “roho isiyokufa” – “immortal soul” – inatuweka kwenye njia panda!

Ujumbe wa kweli, wa kimantiki na thabiti ni bayana : mwanadamu mjinga wa mambo ya Mungu hana chochote cha kutazamia walichoandaliwa wana wa Mungu zaidi ya mimea inayoozeana kila mwaka majira ya baridi.

KRISTO “UFUFUO” – NA HAKIMU

Kristo anajidhihirisha kama njia ya pekee ya ufufuo na uzima, hakimu ya wote walio na wajibu, na mtoa ujira au adhabu atakaporudi tena duniani. Alisema: “Baba amempa mwana hukumu yote” (Yohana 5:22). Tena, Yohana 12:48, kama ilivyokwisha kunukuliwa – “Yeye anikataaye mimi, asiyeyakubali maneno yangu, anaye amhukumuye; neno hilo nililolinena ndilo litakalomhukumu SIKU YA MWISHO.”

Hii ni kanuni ya kimsingi ya imani ya Injili. Paulo (Waebrania 6:1-2) anahusisha hukumu ya milele na ubatizo, ufufuo, n.k kama kanuni (“za kuanza”) za mafundisho ya Kristo. Petro alisema Kristo aliwaagiza wawahubirie watu na kuwashuhudia ya kuwa “ndiye aliyeamriwa na Mungu awe mhukumu wa walio hai na wafu” (Matendo 10:42).

Na Paulo aliwaambia Warumi Mungu amechagua SIKU ambayo (Warumi 2:16)”Atazihukumu siri za wanadamu, sawasawa na injili yangu kwa Kristo Yesu”

Vifungu vifuatavyo vyaonyesha picha ya Biblia kuhusu hukumu ijayo:

“Na kama vile watu wanavyowekewa kufa mara moja, na baada ya kufa hukumu.” (Waebrania 9:27)

“Na wote waliokosa, wenye sheria, watahukumiwa kwa sheria… SIKU ILE Mungu atakapozihukumu siri za wanadamu, sawasawa na Injili yangu” (Warumi 2:12-16).

“Maana SIKU ile itaidhihirisha … kazi ya kila mtu” (1 Wakorintho 3:13)

“Mungu …atamlipa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake” (Warumi 2:5-6)

“Sisi sote tutasimama mbele ya kiti cha Mungu … kila mtu miongoni mwetu atatoa habari zake mwenyewe mbele za Mungu. ” (Warumi 14:10-12)

“Kwa maana imetupasa sisi sote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ili kila mtu apokee ijara ya mambo aliyotenda kwa mwili, kadiri alivyotenda, kwamba ni mema au mabaya”

“Kristo Yesu, atakayewahukumu walio hai na waliokufa; kwa kufunuliwa kwake na kwa ufalme wake.” (2 Timotheo 4:1)

WENGI WAMEITWA, WATEULE NI WACHACHE

Kwa kupitia kwa mahubiri, Mungu “achagua watu katika hao (mataifa)” kwa ajili ya jina lake” (Matendo 15:14), “na kujisafishia watu wawe milki yake mwenyewe, wale walio na juhudi katika matendo mema” (Tito 2:14). Ingawa mwito huu umewaendea watu wa kila namna, taifa, kabila, na wale ambao wameitikia mwito huu baada ya karne nyingi ni wengi, sio wote walioitwa watakaochaguliwa…”Waitwao ni wengi, bali wateule ni wachache” (Mathayo 22:14). Kwa maana wengi wanaolipokea neno hawashawishiki vya kutosha nalo ili kutoa miili yao kama dhabihu iliyo hai, takatifu na ya kumpendeza Mungu (Warumi 12:1). Au kama Paulo alivyowambia Waebrania (4:2) – “Lakini neno lile lililosikiwa halikuwafaa hao, kwa sababu halikuchanganyika na imani ndani yao”

Hii inaonyeshwa dhairi katika mfano wa mpanzi. Mbegu inaangukia udongo wa kila aina. Kama matokeo, inazalisha matunda kiasi gani, inayokubalika na isiyokubalika au hapana tunda lolote (Mathayo 13:23). Hivi kundi kubwa , wanaoishi na waliokufa, kila mmojawapo akiwa ana wajibu mbele za Mungu kulingana na jinsi Mungu anavyowajua. Hatuwezi kumhukumu mtu yeyote kwa mambo haya. Twaweza kufikiria kusudi fulani wataingia Ufalmeni bila shida; wengine, wakataliwe, bali ni Mungu tu ajuaye. Uamuzi ni wa mwenyezi Mungu ambaye ndiye hakimu wa kweli; atakayedhihirishwa na Kristo atakapofunuliwa.

MASWALI YA SOMO LA 12

1. Hukumu kwa kila mtu inafanywa kwa misingi ipi?
2. Nini kilimfanya Adamu akawa ana wajibu mbele ya hukumu ya Mungu?
3. Nini ilikuwa matokeo ya mapuuza ya Adamu na hatima ya matendo yake:
4. Kumhusu yeye?
5. Kuhusu vizazi vyake?
6. Kusudi kuu la Mungu katika uumbaji lilikuwa nini?
7. Wale wasiojua sheria na amri za Mungu watatakiwa kuhukumiwa?
8. Maandiko yapi yanaunga mkono jibu lako?
9. Mtu anafikiaje kiwango cha kuwajibika kwa mapenzi ya Mungu?
10. Ibrahimu alifikiaje kiwango cha kuwa na wajibu mbele za Mungu?
11. Ni kipengele kipi cha Muumbaji kilivutiwa na Sheria za Musa?
12. Nini kilifanya Waisraeli kama taifa kuwajibika mbele za Mungu?
13. Mataifa mengine yaliwajibika vipi mbele za Mungu?
14. Toa vifungu 2 kuthibitisha walio na wajibu mbele za Mungu watajibu kwa ajili ya matendo yao mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo.
15. Je, wote ambao wamepokea mwito wa Mungu watakubaliwa mbele ya kiti cha hukumu?
16. Hukumu itafanyika lini ?